# Kushikilia marekebisho katika mguu kifundo

Muongozo wa uvaaji viatu tiba hatua kwa hatua



Tutatembea na wewe


## KUDUMISHA/KUSHIKILIA MAREKEBISHO YA MATIBABU

- Baada ya awamu ya kufunga muhogo (plaster of Paris), miguu ya mtoto wako itakuwa sawa
- Ni muhimu kutambua kwamba matibabu hayajaisha katika hatua hii
- Mguu kifundo na nafasi kubwa ya kujirudia hadi mtoto wako atakapokuwa na umri wa miaka minne
- Awamu ya kushikilia ni kwa ajili ya kudumisha marekebisho yaliyofanikishwa katika awamu ya kufunga muhogo (P. O. P) ili mguu usijirudie tena
- Baada ya marekebisho ya mwisho ya kufunga mguu kwa Muhogo, mtoto atapatiwa viatu Tiba ili kudumisha marekebisho hayo
- Ni muhimu kufuata maagizo ya namna ya kuvaa viatu ili kuepusha mguu kurudi kwenye ulemavu na mtoto wako akalazimika kuanza matibabu upya tena

## RATIBA YA UVAAJI BORA WA VIATU TIBA


**MWEZI 1/MIEZI 2/MIEZI 3 – MASAA 23 KWA SIKU**

Saa moja lililobakia litatumika katika shughuli mbalimbali mfano: kuoga



**BAADA YA MIEZI 3 MTOTO ATAVAA VIATU TIBA KWA MUDA WA MASAA 14 – 16 KWA SIKU**

Mtoto atavaa viatu tiba kwa muda wa usiku na muda wa mchana akiwa amesinzia/lala



## UVAAJI WA VIATU TIBA KWA WATOTO UTAKOMA BAADA YA MIAKA MINNE (4) NA BAADA YA KUONANA NA MTAALAMU KATIKA KLINIKI YA KUHUDUMIA WATOTO WA MGUU KIFUNDO.





## VIDOKEZO VYA UVAAJI VIATU TIBA



- Mtoto wako atahitaji siku chache ili kuzoea kuvaa kiatu tiba
- Usimvue kiatu tiba iwapo mtoto analia
- Hakikisha uvaaji wa kiatu tiba ni sehemu ya utaratibu wa maisha ya mtoto kwa muda uliopangwa ( mpaka umri wa miaka 4)
- Hakikisha mtoto anavalishwa viatu kwa usahihi
- Kiatu tiba lazima kuvaliwa kila siku kwa muda sahihi
- Viatu lazima vivaliwe vikiwa na kizuizi cha katikati ya mguu na mguu.
- Rekebisha kizuizi cha katikati ya miguu kwa kukisogeza juu na chini na umuonyeshe mtoto namna anaweza kuchezesha miguu akiwa amevaa viatu tiba, pia namna ya kukunja miguu usawa wa magoti akiwa amevaa viatu tiba.
- Mtoto atazoea uvaaji wa viatu tiba kwa haraka
- Usiache kumvalisha mtoto viatu tiba hata kama una changamoto.
- Rudi haraka kwenye kituo cha Huduma za mguu kifundo kama utahitaji msaada zaidi

## NAMNA YA KUTUMIA/KUVAA KIATU TIBA






- Hakikisha usafi na ukavu wa miguu ya mtoto kabla ya kumvalisha viatu.
- Usiweke krimu yoyote kwenye miguu
- Tumia soksi za pamba
- Anza kumvalisha mtoto kiatu tiba mguu ulioathirika zaidi
- Fungua kiatu kabisa kibaki wazi
- Anza kwa kupinda goti na kusukuma chini wakati unavaa kiatu ili kuhakikisha kisigino kinagusa ukuta wa chini wa kiatu
- Mara ya kwanza kuvaa : Chora alama kwa kalamu mbele ya vidole kama mwongozo
- Hakikisha kisigino kiko kimefika mwisho kabisa wa kiatu tiba.
- Bonyeza kidole gumba chako katikati ya mguu ili kushikilia mguu usihame wakati unapofunga kamba.
- Hakikisha kamba za viatu hazijakaza sana lakini pia hazijalegea kushindwa kushikilia mguu katika sehemu sahihi.
- Shikilia kiatu mkononi mwako wakati unavuta goti lililokunjwa juu ili kuhakikisha mguu hauchezi chezi ndani ya kiatu




- Kaza kamba kama mguu haujashikiliwa vyema
- Kwa kupitia tundu dogo lililopo katika eneo la kisigino, angalia kisigino kama kimelala vizuri katika ukuta wa ndani wa kiatu
- Unapaswa kuwa na uwezo wa kuona mstari uliochora mbele ya vidole
- Ikiwa kisigino hakipo au huwezi kuona mstari, ondoa kiatu na anza tena
- Usichoke na usiogope kurudia mpaka ufanikiwe
- Baada ya muda flani itakuwa rahisi kumvalisha mtoto kiatu
- Baada ya siku za kwanza za marekebisho, mtoto wako anapaswa kuwa amevaa viatu tiba vizuri

## KIATU TIBA HAKITAMZUIA MTOTO WAKO KUSHINDWA KUTAMBAA, KUSIMAMA NA KUTEMBEA

## CHANGAMOTO ZA KIATU TIBA





- Ni muhimu sana kuwasiliana na daktari wako au kurudi kliniki ikiwa mtoto wako ana shida yoyote kuhusu kiatu tiba
- Changamoto za kiatu tiba zinaweza kuwa:
  - Kizuizi cha katikati ya mguu na mguu kuwa kifupi sana.
  - Viatu kuwa vidogo
  - Dalili za kujirudia kwa mguu kifundo kuanza kuonekana tena
- Ikiwa kiatu hakitoshei kwa usahihi, kinaweza kusababisha changamoto. Unashauriwa kuwasiliana na kliniki yako mara moja iwapo:
  - Alama nyekundu ya msuguano, vidonda au michubuko miguuni
  - Mguu huteleza/kutoka nje ya kiatu hata kama kamba zimekazwa/umekaza vizuri

## CHANGAMOTO YA MTOTO KUSHINDWA KULALA



Ikiwa, baada ya kuzoea viatu, mtoto wako anashindwa kupata usingizi na hajisikii vizuri au haoti meno, n.k., kuna mambo kadhaa ya kujaribu:

- Angalia viatu bado ni saizi sahihi. Unaweza kuhitaji viatu vikubwa kwa kuwa hivyo vitakuwa vinabana
- Kizuizi cha katikati kinaweza kuwa kifupi sana wakati mtoto wako anakua Ikiwa kizuizi kinaweza kubadilika upana wake inaweza kusaidia
- Hakikisha mtoto anafunikwa na shuka moja au blanketi nyepesi kuongeza utulivu
- Weka kizuizi laini (mfano : taulo au kanga iliyokunjwa) kando ya kitanda ikiwa kiatu tiba kinagonga juu yake na kumuamsha mtoto wako
- Mhamishie mtoto wako mkubwa kwenye kitanda kikubwa ikiwa anahitaji nafasi kubwa zaidi

## MIADI YA KLINIKI



- Kliniki itawajibika kupanga ukaguzi wa mara kwa mara ili kukagua miguu na Viatu vya mtoto
- Usikose ziara hizi za kliniki, hata kama miguu inaonekana sawa
- Idadi ndogo ya watoto wenye miguu kifundo hujirudia wakati mtoto anakua, na hiyo inaweza kuhitaji upasuaji zaidi. Hii ndio sababu ziara za kliniki za kawaida ni muhimu

### Msaada na ushauri

- Kliniki nyingi zina mtu ambaye atatoa elimu kuhusu mguu kifundo na matibabu yake
- Katika siku za kliniki utakutana na wazazi wengine ambao wana watoto na watoto katika hatua tofauti za matibabu ya mguu kifundo. Kuna vikundi na mashirika ya msaada kwa wazazi kwenye mtandao ambayo yanaweza kukusaidia. Ulizia kliniki kwa habari zaidi


**Ukiwa kama mlezi au mzazi wa mtoto, unajukumu muhimu katika mafanikio ya tiba ya mtoto (mguu kifundo). Ukiwa una maswali au wasiwasi, tafadhali wasiliana na mshauri wako wa kliniki au wa wazazi.**

TAARIFA ZA KLINIKI




## UFUNGAJI WA MUHOGO

| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| TAREHE | | | | | |
| ✓ | | | | | |




## UFUNGAJI WA MUHOGO

| | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|
| TAREHE | | | | | |
| ✓ | | | | | |



## KIATU TIBA

| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 |
|---|---|---|---|---|---|
| TAREHE | | | | | |
| ✓ | | | | | |



## KIATU TIBA

| | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 |
|---|---|---|---|---|---|
| TAREHE | | | | | |
| ✓ | | | | | |